

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE

SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA

S.L.P 607

MPIMBWE- KATAVI

Mob 0762 773 954

Tarehe

Kumb Na. MPSS/JI/FORM 1/ 2022.

Jina la Mwanafunzi

.....
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA,
HALMASHAURI YA MPIMBWE MKOA WA KATAVI MWAKA 2022**

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA katika Shule hii Mwaka 2022 Shule hii iko kata ya Kibaoni, Halmashauri ya wilaya ya Mpimbwe Mkoa wa Katavi Muhula wa masomo unaanza tarehe /JANUARI/2022 unatakiwa kufika Shuleni Kuanza masomo tarehe /JANUARI/2022 ukiwa na vifaa vyote vilivyo agizwa katika barua hii. Usichelewe kufika shuleni zaidi ya tarehe

Muda wa kuhudumiwa ofisini ni kuanzia saa 01:30 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

(a) Wavulana: Suruali mbili za blue bahari zinazotosha kiuno zenye marinda mawili (**SURUALI ZENYE MSHONO WA MODAL HAZITAKIWI KABISA**), mashati mawili meupe Yenye mikono mifupi, tai mbili (2) za blue bahari, Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba Visivvo na visigino virefu na Soksi nyeusi jozi mbili. Sweta 1 yenye rangi ya kijani kibichi.

(b) Wasichana: Sketi mbili za blue bahari zenye urefu wa sentimita 26 kutoka kwenye goti au Zaidi, Iwe ya lina box, lina 8, lina moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande wa kushoto. (**SKETI ZIWE NDEFU SANA ZIFIKE KWENYE KIWIKO CHA MIGUU, SKETI FUPI HAZITAKIWI KABISA**), mashati mawili meupe Yenye mikono mifupi, tai mbili (2) za blue bahari.

Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba Visivvo na visigino virefu na Soksi nyeusi jozi mbili.

Kwa wasichana watakao vaa Hijabu ziwe za rangi nyeupe kama mashati yao. Sweta 1 yenye rangi ya kijani kibichi.

(c) SARE ZA MICHEZO

Sare za michezo kwa shule hii ni Tracksuit ya rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana, Tshirt ya blue na Bukta ya Blue kwa wavulana na wasichana. Viatu vya michezo (raba nyeupe)

Kwa wavulana na wasichana.

2.2 VIFAA VYA DARASANI

Unatakiwa kuja na daftari kumi (10) aina ya Counterbook Quire 3 nakuendelea, Mkebe Wa hesabu (Mathematical Set), Rula, kalamu za bluu au nyeusi za kutosha za kuandikia, Kamusi mbili moja ya kiingereza na nyingine ya kiswahili.

MAVAZI YA HOSTEL KWA WASICHANA

- Shamba dress, mshono wa gauni rangi ya kijani (kitambaa cha shuka la kimasai lenye mistari ya drafti ya rangi ya kijani na nyeusi). Mshono wa Soro
- Kila mwanafunzi wa Hostel anatakiwa kuja na kanda mbili, taulo ndefu au kitenge kizito kwa ajili kuogea.
- Shuka mbili za rangi ya Bluu bahari iliyokolea, mto1, blanketi1, na chandarua.
- Godoro moja lenye kipimo cha futi mbili na nusu.
- Tshirt rangi ya bluu yenye nembo ya bendera ya Taifa, jina TANZANIA na mistari ya njano.

NB:Sketi na Gauni(shamba dress) ziwe **ndefu sana**

➤ **MAVAZI YA HOSTEL KWA WAVULANA**

- Suruali mbili nyeusi za kitambaa, zinazotosha kiuno zenye marinda mawili suruali aina ya modal hazitakiwi kabisa.
- Kila mwanafunzi wa Hostel anatakiwa kuja na kanda mbili kwa ajili kuogea.
- Shuka mbili za rangi ya Bluu bahari iliyokolea, blanketi 1, mto 1, chandarua na taulo.
- Godoro moja lenye kipimo cha futi mbili na nusu
- Tshirt rangi ya bluu yenye nembo ya bendera ya Taifa, jina TANZANIA na mistari ya njano.

NB: Wanafunzi wa hostel wakiwa shuleni watatakiwa kuvaa nguo zilizotajwa hapo juu na sio Vinginevyo.

HUDUMA YA AFYA

Unatakiwa kuwa na bima ya afya. Pia kwa wenye mahitaji maalumu ya kiafya watoe taarifa mapema kwa uongozi wa shule ukiwa na uthibitisho wa barua kutoka kwa Daktari ikiwa na muhuri wa kiofisi.

VIFAA VYA USAFI

Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi

- Jembe jipya lenye mpini lililo nolewa vizuri
- Ndoo tatu zenye ujazo wa lita kumi
 - ndoo moja kwa ajiri ya kuogea
 - ndoo ya pili kwa ajiri ya kutunzia maji ya kunywa
 - ndoo ya tatu kwa ajiri ya maji ya usafi wa madarasani na ofisini
- Kwanja moja jipya la dukani lililonolewa vizuri.
- Ufagio wa wima au soft bloom (mmoja)

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama Iliyorekebisha kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote Inayotolewa na Wizara ya Elimu, Teknolojia, Sayansi na mafunzo ya Ufundi yenye dhamana nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yatakayofafanuliwa zaidi utakafika Shuleni:

- a) Utatakiwa kuwaheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
- b) Utatakiwa kuwa na mahudhurio mazuri katika kila shughuli inayofanyika ndani au nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- c) Utatakiwa Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Utatakiwa Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Utatakiwa Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya Mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Utatakiwa Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- g) Utatakiwa Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
- h) Utatakiwa Kuzingatia ratiba za shule wakati wote.
- i) Utatakiwa Kutunza mali za umma, mali zako na za wenzako
- j) Utatakiwa kuwa na Lugha nzuri unapooonga na wenzako au na watu wanaokuzidi umri (Lugha Za matusi, kejeli na maudhi hazitikiwi kabisa)
- k) Utatakiwa kuandika notes, kufanya mazoezi na kufanya majaribio ya kila somo unalosoma.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

- a) Wizi
- b) Uasherati na Ushoga
- c) Kusababisha mimba ndani au nje ya Shule
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuoa au kuolewa
- i) Kupata mimba, Kutoa mimba ndani au nje ya Shule.
- j) Kugoma, kupanga, kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- l) Kuwa na simu au Line ya Simu ya mkononi au kifaa chochote kinachoashiria kuwa na simu.
- m) Ubakaji
- n) Kulala nje ya Shule bila ruhusa.

MAKATAZO MBALI MBALI UTAKAYOTAKIWA KUYAZINGATI UWAPO KATIKA SHULE HII.

- i) Mwanafunzi harusiwi kuvaa kofia, herein, mikufu, kanga, bangili, pete, sketi fupi au za kubana/mipasuo au kuvaa suruali kwa mtepesho. Marufuku kufuga nywele ndefu, kupaka rangi kucha au nywele, kujichubua. Yeyote atakaye patikana na haya atachukuliwa hatua kali.
- ii) Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, radio, kamera, CD, DVD, mshumaa, pasi ya Umeme, Heater na silaha yoyote kama vile kisu au panga. Atakayapatikana na kosa hili atachukuliwa hatua kali sana.
- iii) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mapenzi, kujuhusisha na mazungumzo ya mapenzi, kuingia kwenye vilabu vya pombe, kuingia kwenye kumbi za starehe kama vile kwenye Madisko na Video, kuandika barua za mapenzi au kupokea barua za mapenzi. Atakayepatikana na kosa hilo atachukululiwa hatua kali bila msamaha.
- iv) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa lugha za matusi, kejeli, dharau na kashfa. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu anayemzidi umri akiwa amejishika kiunoni au ameweka mikono mfukoni.
- v) Mwanafunzi kutofanya majaribio au mazoezi au kutokusanya kazi aliyopewa au kutoandika notes (nukuu) alizopewa na mwalimu wa somo ni KOSA KUBWA SANA. Mwanafunzi atakaye patikana na kosa hili atachukuliwa hatua kali kwa kukwamisha lengo lililomleta katika shule hii.
- vi) Mwanafunzi haruhusiwi kuficha taarifa za uovu wowote aliouona au kuusikia. Kupatikana na kosa hili mwanafunzi atachukuliwa hatua kali.

- vii) Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi kitabuni, katka dawati,meza, viti au kwenye kuta za majengo ya shule. Kukaidi kutii katazo hili mwanafunzi atachukuliwa hatua kali sana.
- viii) Ni kosa kwa mwanafunzi kumkimbia mwalimu au mfanyakazi yeyote. Mwanafunzi atakaye patikana na kosa hili atachukuliwa hatua kali za kisheria.
- ix) Mwanafunzi harusiwi kufanya udanganyifu katka mtihani wowota ule, uwe wa ndani au wa nje. Kufanya kosa hili, mwanafunzi atachukuliwa hatua kali sana.
- x) Katika Shule hii kuna vikundi vya dini kama vile TYCS, ASA, CASFETA, UKWATA na TAMSA.Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu kikundi anachosali mwenzake kwa asilimia 100%. Kudharau au kukejeli kikundi anachosali mwenzako kutasababisha uchukuliwe hatua kali za kisheria bila msamaha.
- xi) Wastani wa Shule ni 45% atakayepata chini ya wastani huu atapewa adhabu kali bila msamaha.

TAFADHALI

SOMA KWA MAKINI MAELEZO / MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA UPATE ELIMU, MOTO WA SHULE HII NI;

*** ELIMU NI UKOMBOZI*
NJOO UJIKOMBOE!**

**ALICKO J. KAMINYOGE.
MKUU WA SHULE**

0762773954 – NAMBA YA SIMU YA MKUU WA SHULE

0746420986 – ANIZA MALOBA MAKAMU MKUU WA SHULE

0768186713-ESTHER C. RUHOMWA MWALIMU MLEZI WA WANAFUNZI WA KIKE

0755960647-OSWARD MWAKYUSA MWALIMU MLEZI WA WANAFUNZI WA KIUME

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE
SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA
FOMU YA KUKUBALI NAFASI

A. MWANAFUNZI.

Jina la Mwanafunzi
Anuani
Tarehe.....
MIMI.....
..... Nimekubali kujiunga na Jumuiya ya Shule ya Sekondari Mizengo Pinda.
Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa. Ninaahidi kuwa mtiifu,
nitazingatia Sheria, taratibu zote za Shule kama nilivyozisoma na zingine nitakazo
elelekezwa.
Saini ya Mwanafunzi
Tarehe.....

B. MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

MIMI..... Ambaye ni
mzazi/mlezi wa mwanafunzi anayelitwa
..... Nimesoma kwa makini maagizo
ya Shule ya Sekondari Mizengo Pinda yaliyotolewa yanayohusu mtoto wangu.
Nimekubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo ya thamani aliyopewa na serikali.
Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza, kumlea na
kumhudumia kwa kadiri ya wangu ili kuhakikisha kuwa anahitimu masomo yake kwa
mafanikio kielimu na kitabia.
Saini ya Mzazi/Mlezi.....
Tarehe.....

KUMBUKA:

Hakikisha mwanao haji na simu Shuleni. Akipatikana na simu shuleni atafukuzwa shule.

HII NI AMRI YA SERIKALI.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MPMBWE DISTRICT COUNCIL
MIZENGO PINDA SECONDARY SCHOOL
STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM

TO THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE

.....
.....
.....
.....
.....

Please examine the under named student and note any medical complications towards her joining this school.

Student's name..... Age

..... Class

1) Blood (any infection noted)

.....
.....
.....

2) Blood group

.....

3) Stool

4) Urine Analysis

.....
.....
.....

(Note pregnancy for girls)

5) Eyes (any eye defect)

.....
.....

6) Ears (hearing strength)

.....

7) Chest

8) Heart diseases

.....
Any chronic complains which needs attention of the School Authority

.....
.....

Name of the Medical officer

Designation Signature

Station Date Official Stamp

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE
SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA

FORM YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili la mwanafunzi kama ilivyotumika katika mtihani wa darasa la VII
.....
 2. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi. Tarehe..... mwezi.....mwaka.....
 3. Mahali alipozaliwa mwanafunzi.
 - i. Kitongoji.....
 - ii. Kijiji.....
 - iii. Kata.....
 - ii. Wilaya.....
 - iii. Mkoa.....
 4. Kabila la mwanafunzi.....
 5. Jinsia ya mwanafunzi.....
 6. Dini yake.....
 7. Jina la baba yake..... Nambari ya simu
 8. Jina la mama yake..... Nambari ya simu
 9. Kamam analelewa na mlezi, Jina la mlezi.....
Uhusiano na mwanafunzi.....
Nambari yake ya simu.....
 10. Jina la Ndugu/Jirani kimakazi.....Namba ya simu.....
 11. Shule ya msingi alikotoka mwanafunzi.....
 12. Jina la mwenyekiti wa serikali ya mtaa.....
Nambari yake ya simu.....
 13. Je ana amgonjwa sugu? Kama ndio taja.....
Anatibiwa hospitali gani.....
- Jina la mzazi.....Saini.....
- Tarehe.....